

LEARNING BY EAR

"If a tree falls... - Deforestation in Africa"

EPISODE ONE: "Trees and rainfall"

AUTHOR: Romie Singh

EDITORS: Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz

PROOFREADING: Natalie Glanville-Wallis

List of characters EPISODE ONE:

Narrator

SCENE 1 Isingoma (Isi) (m, 18)

SCENE 2 Akiki (f, 7) Isi (m,18)

SCENE 3 Chika (f, 18)

SCENE 4 Talib (m, 20) Boys/Men Group Mulogo (m, 22) Isi (m, 18) Akiki (f, 7)

SCENE 5 Talib (m, 20) Chika (f, 18)

SCENE 6 Isi (m, 18) Akiki (f, 7)

INTRO:

Karibu katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha yako*, na mchezo wetu mpya wa redio uitwao, “Mti unapoanguka.....” ulio na sehemu kumi. Kisa hiki ambacho kinatukia kwenye mazingira ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, kinazungumzia jinsi uharibifu wa misitu ulivyoathiri vibaya maisha ya vijijini na kusababisha mgogoro kati ya jamii mbili zinazoshughulika na kilimo. Kwa sasa hivi, watu hao ambao wanaishi kama wakimbizi katika kambi ya Dovani wameanza kupata ufumbuzi wa jinsi ya kukabiliana na mustakabali wao.

Bara la Afrika ndilo bara la pili kwa kasi ya uharibifu wa misitu duniani ambapo takriban asilimia 90 ya wakazi wake hutumia kuni kupikia. Hali hii inachangia ongezeko la joto duniani na kusababisha kuharibika kwa mazao yetu ya chakula, kuangamia mifugo yetu na maisha yetu kutatizika.

Mchezo wetu “Mti unapoanguka..” unaangazia masuala kama nishati mbadala na njia nyingine za kilimo zinazolenga kulinda misitu yetu na kutatua mizozo. Kijana Isingoma na mama yake wamenusurika kwenye vita na wanakaa katika kambi ya Dovani. Lakini jamaa zao wengine wako wapi? Ungana nasi wakati Isi anapotueleza kuhusu maafa yaliyomfika pacha mwenzake Kato.

Episode One: “Trees and Rainfall.”

1. MUSIC UP

Scene 1

1a. SFX: Outside: evening noises. Crickets, cows

2. ISI NARRATOR: Jina langu ni Isingoma. Watu huniita Isi kwa kifupi. Nina umri wa miaka 18. Nina kaka na jina lake ni Jamal na pia nina ndugu, pacha mwenzangu tunayefanana sana, aitwaye Kato. Mimi na yeye hulka zetu daima ni kama za mtu mmoja. Lakini tangu vita vilipoanza hatujaonana...

3.SFX: War/gunshots, distant screams/shouting/running through bushes.

... Niliita, 'Baba, Kato, Jamani? Mko wapi? Lakini sikusikia chochote ila milio ya risasi na mayowe. Baadaye niligundua kwamba wanaume wengi na wavulana wengi walikuwa wametekwa nyara na kulazimishwa kujiunga na waasi. Mimi na mama yangu tulibahatika kukimbia. Baba yangu ni Chifu wa wilaya yetu, Banega. Mamangu anamtamani sana- sisi sote tunamtamani- Alikuwa... angali... kiongozi wa jamii yetu. Lakini ninamlilia ndugu yangu Kato. Tulikuwa na uhusiano mzuri sana. Najihisi nimepungukiwa kwa kumkosa ndugu yangu. Nataka tuwe pamoja huko aliko. Lakini yuko wapi?

Scene 2

3a. SFX Evening ambience outside

4. Isi hums a sad song while he looks after the cows

- 5.AKIKI: (softly)** Isi? Usiku unaingia. Hutaki kupeleka ng'ombe nyumbani sasa?
- 6.ISI:** Aaha, Vipi Akiki! Ng'ombe bado wanakula.
- 7.AKIKI: (sighing)** Una bahati kama nini! Kuna nyasi za kuwatosha ng'ombe karibu na kambi. Mimi nimetembea mchana kutwa nikitafuta kuni. Tazama! Nimepata hizi kiasi kidogo tu.
- 8.ISI:** Tumekuwa katika kambi hii ya Dovani kwa muda gani sasa, Akiki? Miezi sita? Na kwa muda wote huo eneo kubwa la misitu na nyasi limeharibiwa. Hayo yanatendeka kila mahali!
- 9.AKIKI: (stammers over long words)** Mama yako ni mwanachama wa ka....kama..t...i. Huwa wakizungumzia jinsi ya kurekebisha hali ya mambo.
- 10.ISI:** Ni mama yako pia Akiki. Wewe dadangu mdogo!
- 11.AKIKI:** Naaam. Humsikia akilia usiku. Na wewe je?
- 12.ISI:** Mimi pia, lakini kazi yake kuhusu misitu humuondolea fikra kuhusu babangu na ndugu zangu. Na vipi jamaa zako? Sesi dadako mkubwa? Natumaini walipata mahali pa kukimbilia.
- 13.AKIKI:** Sesi na mama walikimbia. Nadhani waasi walimteka babangu.
- 14.ISI:** Babangu pia. Na Kato. **(Sighs)** Sijui yuko wapi. Zamani nilikuwa nikijua anakokwenda na alichokifikiria. Lakini sasa simhisi hata kidogo. Nahisi kama sehemu yangu moja imeangamizwa. Unajua watu wanavyosema kuhusu watoto mapacha?

15.AKIKI: Hapana! Kwani unasemaje?

16.ISI: Ati sisi mapacha kama kisu kikatacho pande mbili. Tuna uwezo wa kuwadhuru wanaotudharau. Tuombe Mungu kwamba Kato atasababisha hao waasi washindwe vita ili tupate amani.

17.AKIKI: Amiin! Njoo- Twen'zetu kambini. Mama yetu anahitaji hizi kuni kupikia.

18.MUSIC UP

Scene 3

18a. SFX Early morning ambience outside: birdsongs, cattle

19.CHIKA NARRATOR: Jina langu ni Chika. Leo nimetimia umri wa 18. Mimi na Talib ni viongozi wa vijana wa kundi la *Saidia Afrika*. Tumeletwa kufanya kazi hapa kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani. Mimi natoka kwenye milima ya kaskazini na Talib anatoka maeneo kame ya magharibi. Tunawafunza vijana namna nzuri ya kuyatunza mazingira yetu na pia jinsi ya kunufaika na kilimo pamoja na misitu. Tumeona jinsi ardhi inavyoendelea kuwa kame kwa kasi ya kutisha. Ukataji miti- ni tatizo sugu. **(GIVES A BIG SIGH)** __Hah! Dovani ni kambi ya wakimbizi iliyojengwa vizuri. Kutokea hapa juu nilipo ninaweza kuona mapaa ya nyumba. **(SHORT PAUSE)** Wakati ndo huo! Ebu nijiandae niondoke. Ninafanya kazi pamoja na kundi la wanawake. Tuliunda kundi hilo ili wanawake wahusishwe zaidi kusimamia chakula kambini. Hata hivyo wao ndio wapishi! Asubuhi ya leo tumeamua kupanda maharagwe aina ya soya. yasoyasoya. Talib naye pia yupo. Ni wakati wa mazungumzo kwenye kundi la wanaume.

Scene 4

19a. SFX OUTSIDE / HAND BELL

21.TALIB: (OFF MIC) Njoooni! Mkutano wa vijana wa kiume unaendelea sasa! Tafadhalini tukutane chini ya mkuyu. Mje na kalamu na karatasi.

22. Background voices of boys and men

23.TALIB: Hamjambo! Nafurahi kuona kwamba leo tumekuja wengi. Tafadhalini kaeni kwenye kivuli.

24.BOYS/MEN: Hatujambo Talib.

25. Low chatter as they sit down

26.TALIB: Haya basi. Natumai mmeshauriana baina yenu na pia na wazee wenu na mmesoma taarifa zilizo kwenye maktaba ya afisi yetu. Mlipewa jukumu la kuchunguza jinsi mvua inavyotokea.

27. MURMUR OF YES

28.TALIB: Haya ! Tuangazieni mchoro huu. Ni mchoro unaohusu hali ya hewa: Hapa upande wa kulia mnaona jinsi mito inavyoelekeza maji yake kwenye maziwa na hatimaye kwenye bahari. Upande wa kushoto kuna milima yenye misitu na juu kuna mawingu angani. Na hapa juu kulia, mvua inanyesha kurudi kwenye mito na baharini. Sawa? Sasa! Nani atatufafanulia zaidi kuhusu mchoro huu? Mvua huja vipi?

29. BOYS GROAN AND GIGGLE

30.MULOGO: Jua linatia joto kwenye maji ya bahari, maziwa na mito. Joto hilo huvukiza maji. Maji hugeuka kuwa mvuke.

- 31.TALIB:** Sawa. Asante Mulogo! Hapo unaona mvuke. Mvuke huo huchanganyikana na hewa...kisha? Naam Isi.
- 32.ISI:** Mvuke wenye joto hupaa kwenye tabaka za juu za hewa ambazo ni baridi zaidi, kisha mvuke huo hupata baridi. Mawingu yanaanza kuonekana.
- 33.TALIB:** Maanake?
- 34.MULOGO:** Mvuke hubadilika kuwa maji. Ni kama unapopumulia glasi, hewa ya joto ya pumzi zako hukumbana na glasi ya baridi na kugeuka kuwa maji.
- 35.TALIB:** Umeeleza vizuri Mulogo! Mvuke hugeuka kuwa matone ya maji.
- 36.ISI:** Na kwenye mawingu, matone hayo madogo huendelea kuwa makubwa yanapojiongezea unyevu zaidi..
- 37.TALIB:** Vizuri Isi. Halafu?
- 38.BOYS CALLING OUT:** Mimi...Mimi...Ninajua
- 39.TALIB:** Shhh. Akiki? Kwani leo umekuwa mvulana?
- 40. BOYS GIGGLE**
- 41.TALIB: (gently)** Unafanya nini hapa? Unatakikana kuwa pamoja na wasichana wenzako.
- 42.AKIKI:** Tafadhali Talib. Ninataka kuwa pamoja na Isi.
- 43.TALIB: (gently)** Hakuna shida! Karibu! Sasa? Unalo jibu? Tunapata mvua vipi?
- 44.AKIKI: (talking slowly)** Matone yanakuwa makubwa sana.. hivi kwamba ni ...mazito... sana na yanaanguka ardhini...yakiwa mvua..

45. LAUGHTER

46.TALIB: Asante Akiki. Vizuri sana! Maji hupaa yakiwa mvuke...mvuke unageuka matone kisha matone hayo yanakuwa mvua.

47.MULOGO: Kisha mvua inajaza bahari na kupata tena joto, mvuke unapaa na kadhalika na kadhalika! Hivyo ndivyo tupatavyo mvua!

48.TALIB: Sawa...Lakini kweli tungetaka kila wakati maji yetu yageuke kuwa mvuke? Isingoma.

49.ISI: Hapana, si kila wakati. Tunapaswa pia kuhifadhi maji ya mvua kwa matumizi yetu binafsi– kwa mfano kwenye magari yaliyo karibu na nyumba zetu.

50.MULOGO: Hayo hayatoshi. Ni lazima tufyeke misitu tujenge mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji.

51. BOYS MURMUR

52.AKIKI: Talib, tulikuwa na bwana la maji. Lilikuwa limejaa maji ya mvua na tulikuwa tukitumia maji hayo kwa miezi mingi kwa sababu lilikuwa limezingirwa na likipata vivuli vya miti. Wakati Chifu Kipko alipokata ile miti, dimbwi hilo lilikauka maji.

53.ISI: (embarrassed) Naam...wajua... Kampuni moja ya mbao ndiyo iliyomuomba babangu kufanya hivyo. Nadhani watu wetu wanasikitika kwamba dimbwi hilo lilikauka, lakini...

54.MULOGO: Madimbwi! Kama kwamba yanatosha. Ondoa mawazo hayo duni.

55.TALIB: Sawa Mulogo. Jambo la kuzingatia hapa ni MITI na mvua.

56.ISI: Ninavyoelewa mimi Talib, kadiri tunavyopanda miti mingi, ndivyo tunavyopata mvua nyingi. Hasa hapa kwetu..

57.MULOGO: (angry) Zungumza mambo yanayoweze kana Isi. Kwani huoni jinsi ardhi ilivyo kavu? Miti gani ambayo itanawiri hapa?

58.TALIB: Mulogo tafadhali-kumbuka masharti yetu: fikra zote zinafaa. Inatupasa kuheshimu fikra za wenzetu.

59.MULOGO: Naam. Samahani, lakini tunapaswa kuwa na fikra pevu zaidi ya kuzungumzia vidimbwi!

60.TALIB: Tuizungumzie miti. Nani ataeleza kwa nini tunahitaji miti?

61.AKIKI: Ng'ombe wangu anapenda kukaa kwenye kivuli. Mti unamkinga kutokana na jua kali.

62. LAUGHTER

63.TALIB: Hapana! Lakini Akiki amesema sawa! Miti hutukinga sisi na wanyama wetu kutokana na jua kali na pia upepo mkali. Kuna sababu nyingi zaidi za kutufanya sisi tuilinde miti yetu. Tafadhalini kaeni kwenye makundi mjadiliane. Tutasikiliza maoni yenu hivi punde.

64. BOYS MURMUR IN BACKGROUND

65.TALIB: Mulogo? Ebu njoo hapa tungumze tafadhali.

66.MULOGO: Naam?

67.TALIB: Ninaelewa jinsi unavyotatizika Mulogo.

68.MULOGO: Kweli?

69.TALIB: Nadhani! Katika kambi hii tuna fursa ya kubadilishana mawazo na kupata njia nyingine za ufumbuzi wa masuala. Ni fursa adimu hii.

70.MULOGO: Lakini hutupatii nafasi kujieleza na hayo mawazo yako ya ufumbuzi wa kienyeji! Tazama dunia yote hiyo nje. Tunapoteza fursa muhimu...kujiendeleza... kufanya biashara...kupata fedha.

71.TALIB: Lakini hakuna ufumbuzi wa moja kwa moja. Unaona madhara ya ukataji miti. Si kila tatizo ambalo linaweza kutatuliwa kwa fedha.

72.MULOGO: Ewe! Unazungumza kama mzee!

73.TALIB: (Laughing)Na mimi ni mdogo wako kwa umri. Wala si suala la umri. Ni suala la kutafuta ufumbuzi unaotuhusu sote. Siku moja mtarejea vijijini kwenu. Mnatakikana kujiandaa vilivyo kuenda kujenga jamii zetu tangu mwanzo kwa kutumia fikra mpya mtakazojifunza hapa.

74.MUSIC UP

Scene 5

74a. SFX Walking on gravel/sand / Evening sounds

75.TALIB: Lo , Chika! Mulogo kijana mdogo lakini haambiliki. Chifu Apaloo yuko tayari kuelezwa mambo mapya lakini mwanawe hasikii.

76.CHIKA: Labda nimwalike Mulogo ajiunge nasi ajionee mambo yanavyokuwa misitu inapoharibiwa. Anatakikana kuhusishwa zaidi. Ana kipaji cha uongozi kama baba yake.

77.TALIB: Naam, lakini baba yake anapenda sana kuhifadhi mazingira. Anapenda misitu ilhali Mulogo anapinga juhudi kama hizo za babake. Mulogo anataka misitu itakayoleta faida ya kibiashara, kama alivyokuwa akipenda Chifu Kipko.

78.CHIKA: Kweli babake Isi alisababisha matatizo makubwa alipoipa nafasi kampuni ya mbao. Machifu wote wawili walikuwa na mzozo kuhusu haki za ardhi na malisho.

79.TALIB: Ndiyo. Nadhani Isingoma anahisi vibaya kwa hatua ya babake na madhara ya kimazingira iliyosababisha.

80.CHIKA: Lakini mamake ni mzuri. Bi Kipko amejitolea kwa dhati kwa kazi inayotekelezwa na kamati ya kina mama ya misitu.

81.TALIB: Vizuri hivyo. Bwana wee! Yatosha sasa kuhusu kazi! Ni sikukuu yako ya kuzaliwa! Kuna pombe ya mtama afisini inayokusubiri wewe!

82.CHIKA: (laughing) Aakh! Siwezi kunywa pombe hiyo! Nipe glasi ya maji meupe! Nahiari maji zaidi!

83.MUSIC UP

Scene 6

83a. SFX Late evening sounds (quiet ambience with some crickets and animals in background)

84.ISI (humming softly) Aaah Kato, ndugu yangu. Naimba wimbo tunaoupenda. Je unanisikia? Unanisikia? Nionyeshe ishara ndugu yangu!

85.AKIKI: Nifundishe huo wimbo Isi. Labda dadangu pia atausikia.

86.MUSIC UP

OUTRO.

"Mti unapoanguka..." ni mchezo ulioandikwa na Romie Singh.

Na huo kwa leo ndio mwisho wa *Noa Bongo Jenga Maisha Yako*, mchezo wetu mpya wa redio unaoangazia hatari zinazokabili jamii zetu, na sayari yetu, endapo hatutaokoa miti zaidi.

Tafadhali ungana nasi kwenye kipindi cha pili ambapo Mulogo na Isi wanabishana kuhusu jinsi ya kutatua matatizo yanayosababisha mabadiliko ya hali ya hewa.

Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena au kuwatanabahisha wenzako kuhusu kipindi hiki, tafadhali tazama wavuti wetu www.dw-world.de/lbe

Kwaheri kwa sasa!

END OF EP.1